TANGAZO LA SERIKALI NA. 22 la tarehe 17/02/2017

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)

(SURA YA 287)

# SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya Kifungu cha 153(1)*

SHERIA NDOGO ZA (USAFI WA MAZINGIRA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MALINYI ZA MWAKA 2017

Jina na mwanzo wa kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za (Usafi wa Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Malinyi za Mwaka 2017 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Malinyi.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo-

"*Afisa Mwidhiniwa*" maana yake ni Afisa yeyote atakayeteuliwa na Halmashauri kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

"*Afya*" maana yake ni hali timilifu ya kimwili, kiakili na kijamii;

"*Chakula*" maana yake ni kitu chochote kinatumika kwa kuliwa na kunywa na binadamu kujumuisha kitu chochote kinachotumika katika matengenezo ya chakula, kitu chochote kinachoongeza ladha ya chakula, au kitu chochote kinachobadili rangi ya chakula isipokuwa madawa;

"*Choo bora*" maana yake ni choo chochote cha maji chenye sakafu, banda imara la kudumu, limeezekwa, lina mlango imara, bomba la kutolea hewa chafu na lenye mfuniko kwenye tundu la choo na shimo salama na safi kwa ajili ya kutupa kinyesi na mkojo wa binadamu, lililojengwa kwa vifaa vya kudumu, lenye vipimo vya futi 4 x 3 na kimo cha futi 12 na zaidi;

"*Choo cha Umma*" maana yake ni choo kilichojengwa na Halmashauri au wakala wake kwa matumizi ya umma;

"*Eneo la wazi*" maana yake ni eneo lililoachwa kama eneo la mapumziko kwa umma au viwanja vya michezo au kwa ajili ya shughuli zozote ambazo sio ujenzi wa kitu chochote;

"*Halmashauri*" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Malinyi;

"*Hati ya usafi*" maana yake ni hati itakayotolewa na Afisa Mwidhiniwa inayothibitisha kukaguliwa kwa maeneo yote yaliyotajwa katika Sheria Ndogo hizi kulingana na Kanuni za Afya.

"*Kaya*" maana yake ni familia ya watu akiwemo baba, mama, mtoto au watoto na mtu mwingine yeyote anayeishi na familia hiyo, au watu wanaokaa katika nyumba moja na kuishi kama familia au mtu yeyote anayeishi peke yake katika chumba au nyumba;

"*Kero au chukizo*" maana yake ni kitu chochote ambacho kipo katika hali yoyote iwe kinatumika, kimewekwa, kimejengwa, au ni

kichafu kiasi cha kusababisha hatari kwa viumbe na maisha ya binadamu, harufu mbaya na kuudhi, kuzaliana kwa wadudu na wanyama hatari kama vile nzi, mende, sisimizi, panya, nyoka, nyuki, kunguni au aviumbe wengine hatari, mlipuko wa magonjwa au kusababisha madhara ya afya kwa binadamu, na viumbe wengine;

"*Kituo cha taka*" maana yake ni kizimba au ghuba ya taka kilichowekwa na Halmashauri kwa madhumuni ya kuweka taka ngumu kabla ya kusafirishwa hadi kwenye dampo la taka ngumu la Halmashauri;

"*Maji taka*" maana yake ni sawa na ile iliyotajwa katika Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 kuwa ni pamoja na taka zinazotokana na kinyesi, mkojo na jasho, uchafu wa majimaji kutoka majumbani, Taasisi, majengo ya biashara na viwandani;

"*Mimea marefu*" maana yake ni mazao au mimea inayozidi sentimita 15 kwenda juu kama vile Mtama, Mahindi, Mbaazi, Uwele na mengine yote yale yanayofanana na hayo isipokuwa miti;

"*Mkazi*" maana yake ni mtu yeyote anayeishi katika eneo la Halmashauri na ambaye ana kaya au anaishi katika kaya au taasisi iliyopo katika eneo la Halmashauri.

"*Mmiliki*" maana yake ni mtu yeyote ambaye ana miliki ardhi, sehemu za starehe, nyumba za kulala wageni, nyumba za kuuzia vyakula,

kumbi za starehe, mpangaji, wakala wa mpangishaji wa nyumba au jengo na makazi yoyote katika mtaa, endapo mazingira husika ni mtaa au barabara za mtaa;

"*Mkurugenzi*" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri au Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"*Mzalishaji wa taka ngumu*" maana yake ni Mtu yeyote, kaya, Taasisi, biashara, kiwanda ambacho katika kufanya shughuli zao huzalisha taka;

"*Pipa la taka*" maana yake ni chombo chochote chenye mfuniko kinachoweza kuhifadhi taka ngumu zinazozalishwa majumbani, sehemu za biashara, maofisini ili zisisambae na kuchafua mazingira;

"*Taka*" maana yake ni sawa na ile iliyotajwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, 2004 kwamba kitu chochote kimiminika, kigumu, gesi na mionzi, kinachotoa harufu mbaya, au kilichohifadhiwa katika mazingira ya hali ya ujazo, uozo au hali nyingine yoyote inayosababisha uharibifu wa mazingira, ambayo inajumuisha taka;

"*Taka Ngumu*" maana yake ni sawa na ile iliyotajwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, ya Mwaka 2004 kuwa ni taka ambazo haziko katika majimaji kutoka majumbani, katika majengo ya biashara, viwandani na kutoka katika shughuli za kilimo, pamoja na taka za vyakula, karatasi plastiki au taka laini zinazotokana na ujenzi au

ubomoaji majengo utengenezaji bustani na shughuli za uchimbaji madini, mizoga ya wanyama na mabaki ya magari mabovu (scraps);

"*Taka za Majumbani*" maana yake itajumuisha mabaki ya chakula, maganda ya matunda, majivu, kinyesi cha mifugo, taka za bustani, marapurapu ya nguo, karatasi za aina mbalimbali na vitu vingine ambavyo baada ya kuvitumia hutupwa;

"*Taka za Viwandani*" kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004, kuwa ni uchafu unaotokana na uzalishaji viwandani au uchafu usiotokana na uzalishaji viwandani ambao ni chanzo cha nishati, maji, mimea iliyotiwa dawa, au mawasiliano, pamoja na taka nyinginezo ngumu kama zilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, 2004 sehemu ya IX;

"*Uchafu Hatari*" kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Mazingira Na 20 ya mwaka 2004, kuwa ni kitu chochote kigumu, chenye majimaji, gesi au taka zitokazo viwandani, au mafuta machafu, ambayo yanaleta athari za kikemia, kwa binadamu au mazingira;

"*Uchunguzi wa Afya*" maana yake ni hali ya Mtu kupima afya yake kwa kuchukuliwa vipimo vya ndani na nje ya mwili ili kubaini kuwepo kwa vijidudu vya magonjwa vinavyoweza kuleta maambukizi kwa watu wengine;

Wajibu wa kufanya usafi wa mazingira

4. Itakuwa ni wajibu wa kila Mtu, Taasisi au Asasi yeyote kuweka mazingira safi na salama wakati wote na kwa

kuhakikisha kwamba-

(a) Mazingira yanayozunguka eneo lake la makazi au biashara yanakuwa safi wakati wote;
(b) Anaweka na kutumia chombo cha kukusanyia taka za aina zote;
(c) Anachangia gharama za uzoaji wa taka kwenye eneo lake;

Kushiriki shughuli za usafi wa mazingira

5. (1) Kila siku ya Jumamosi ya kila wiki au siku nyingine yoyote itakayotangazwa na Halmashauri itakuwa ni siku ya Wananchi kushiriki katika shughuli za usafi wa mazingira kwa umma katika maeneo yote ya mamlaka ya Halmashauri na atakayeshindwa atakuwa ametenda kosa;

(2) Kifungu kidogo cha (1) hakiathiri wajibu wa kila Mmiliki wa nyumba au Kiwanja au eneo lolote kufanya usafi katika eneo lake mara kwa mara.

Utupaji wa taka

6. (1) Halmashauri itahamasisha na kukagua kila eneo la Makazi au Biashara limeweka miundo mbinu na vifaa vya kutupia taka;

(2) katika maeneo yenye Watu wengi ambapo uzalisha taka uko kwa wingi, Halmashauri itaweka utaratibu maalum wa kutupa na kuzoa taka ambapo wazalisha taka watawajibika kugharamia huduma za uzoaji taka kwa mujibu wa viwango vilivyowekwa na Jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi.

Kutiririsha maji taka

7. Haitaruhusiwa kutitirisha au kuelekeza maji, kutoka vyooni, bafuni, karoni, viwandani, kwenda barabarani, uchochoroni, mtoni, kwenye vyanzo vya maji, maeneo ya wazi, mfereji wa maji ya mvua au sehemu yoyote isiyotengwa kuhifadhi maji taka.

Uendeshaji wa viwanda

8. Ni marufuku kuendesha shughuli za karakana, mashine ya kusaga, kuranda mbao, kukamua maji ya matunda, kuchomelea vyuma au kuendesha shughuli zozote za viwandani zinazozalisha maji machafu, vumbi, kelele au harufu mbaya, uchafu ambao unaleta athari kwa binadamu na viumbe wengi katika maeneo ya makazi ya watu bila kuzingatia taratibu za ujenzi.

Kupanda miti

9. (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kupanda au kuotesha mazao au mimea mirefu katika maeneo ya mjini pamoja na maeneo mengine yaliyozuiliwa na Halmashauri isipokuwa kupanda miti;

(2) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1) hapo juu, Kila Mmiliki wa Eneo atatakiwa kupanda na kutunza angalau miti mitano (5) ili kuboresha mazingira;

(3) Ni wajibu wa kila Mtu kulima ua kufanya shughuli nyingine za kibinadamu kwa kuzingatia taratibu za kuhifadhi mazingira ikiwa ni pamoja na kutokata miti ovyo, kutolisha mifugo katika maeneo yenye mmomonyoko wa udongo, kulima kwa njia ya matuta au kutumia mbinu yoyote ya uhifadhi wa mazingira.

Udhibiti wa mifugo

10. (1) Halmashauri itatenga maeneo maalum kwa ajili ya kulishia mifugo na shughuli za kilimo;

(2) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuacha mifugo au kusababisha mifugo kuzurura ovyo mitaani, kuchunga kwenye vyanzo vya maji, kwenye eneo la barabara, Hifadhi ya barabara, au kwenye eneo lolote lisiloruhusiwa.

(3) Mifugo itakayokamatwa kwa kosa la kuzurua au kuchungwa katika maeneo yasiyoruhusiwa itatozwa faini ya shilingi elfu moja (1000/=) kwa kila Mbuzi,

Kondoo, au Nguruwe na shilingi elfu tano (5000/=) kwa kila Ng'ombe, Punda au Ngamia.

Ilani ya kuondoa kero

11. (1) Endapo Afisa Mwidhiniwa atagundua kuwepo kwa eneo kero yoyote atatoa ilani ya siku saba (7) kwa Mmiliki wa nyumba, Mpangaji, Mtumiaji, na/au Mtu yeyote anayesababisha kuwepo kwa hiyo kero akimtaka kuondoa kero hiyo;

(2) Mtu yeyote atakayeshindwa kutekeleza masharti ya ilani aliyopewa ndani ya muda ulioainishwa kwenye ilani atakuwa ametenda kosa;

(3) Endapo Halmashauri italazimika kuondoa kero hiyo, gharama za kuondoa kero hiyo zitalipwa na Mmiliki kabla au baada ya kuondoa kero hiyo.

Wajibu wa kujenga na kukitumia choo

12. Itakuwa ni wajibu wa kila Mmiliki au Mpangaji wa nyumba ya makazi au Nyumba ya Biashara kuhakikisha kwamba nyumba yake ina choo safi, imara na madhubuti kwa matumizi ya Wakazi wa nyumba hiyo na kuhakikisha kinatumika wakati wote.

Umbali wa kujenga choo

13. Choo kinatakiwa kijengwe umbali wa mita sitini (60) kutoka kisima au chanzo chochote cha maji kinachotumika kwa matumizi ya Nyumbani.

Vyoo vya umma

14. (1) Halmashauri inaweza kumruhusu Mtu yeyote, vikundi vya watu au Taasisi kujenga vyoo vya Umma (Public toilets) katika maeneo ambayo Halmashauri itaona kuwa kuna haja ya kufanya hivyo;

(2) Vyoo hivyo vitamilikiwa na Halmashauri au kwa ubia na wajenzi na vitakuwa ni vya kulipia kama itakavyokuwa imeelekezwa na Halmashauri katika Mkataba na Wakala wake watakaopewa kusimamia

vyoo hivyo.

Vyoo katika maeneo ya mikusanyiko ya Watu

15. Mtu yeyote, Kikundi, au Taasisi yenye lengo la kukutanisha watu wengi kwa wakati mmoja au Mmiliki hoteli, migahawa au kilabu cha pombe, kanisa misikiti, au Mtu yeyote anayemiliki wa jengo linalotumiwa na watu wengi atatakiwa kujenga choo kitakachotofautisha matumizi kwa kuzingatia jinsi.

Maegesho na Matengenezo ya magari mabovu

16. (1) Ni marufuku kwa Mtu yeyote kuegesha, kuosha, au kutengeneza gari, pikipiki au mitambo mibovu kwenye eneo la barabara, hifadhi ya barabara, njia ya waenda kwa miguu, mtaa, eneo la wazi au eneo lolote ambalo halikutengwa kwa shughuli hiyo.

(2) Matengenezo ya magari, pikipiki na mitambo yatatakiwa kufanyika kwenye karakana, gereji au maeneo yaliyoruhusiwa baada ya kupata kibali rasmi kutoka Halmashauri.

Wajibu wa kuondoa na kudhibiti mazalia ya mbu.

17. Itakuwa ni wajibu wa mmiliki wa nyumba kuhakikisha kuwa hakuna mkusanyiko wa maji, maji machafu, takataka au kitu chochote cha majimaji au kigumu ambacho kinaweza kuruhusu kuwepo kwa mazalia ya mbu au wadudu wengine wenye madhara kwa afya ya binadamu.

Upulizaji dawa za kuua Wadudu

18. (1) Mtu yeyote atakayetaka kupulizia dawa za kuuwa Wadudu au wanyama waharibifu ***(Fumigation)*** katika nyumba yoyote au mahali popote atalazimika kuomba kibali cha kufanya shughuli hiyo kutoka Halmashauri.

(2) Halmashauri itajiridhisha kwanza kwamba tahadhali zote zinazoweza kuathiri uhai wa viumbe hai wengine zimechukuliwa, na Mtu huyo anao utaalamu wa kupulizia dawa za kuuwa wadudu au

Wanyama waharibifu.

Uendeshaji wa Hoteli, Hosteli na Shule

19. (1) Itakuwa ni wajibu wa kila Mmiliki wa nyumba za kulala wageni, Mgahawa, Hoteli, Hosteli, Shule au Nyumba za biashara kuhakisha anapata kibali cha afya baada ya kukaguliwa na kuonekana kuwa amekidhi masharti ya afya kutoka Halmashauri kabla hajaanza kutoa huduma.

(2) Kibali kitatolewa baada ya Halmashauri kujiridhisha kuwa-

(a) upo mwanga na hewa ya kutosha katika eneo la biashara;
(b) tahadhali ya moto na dharura nyingine;
(c) nafasi na vifaa (samani ) za kutosha;
(d) uimara wa jengo;
(e) kuna mfumo imara wa maji taka, na maji safi, na uhifadhi wa taka ngumu;
(f) kuna vyoo na mabafu safi vya kutumika wa jinsi zote; na
(g) kama ujenzi wa jengo umezingatia watu wenye mahitaji maalumu hasusan Walemavu.

Upimaji wa afya za Wahudumu

20. (1) Kila baada ya miezi mitatu (3), Halmashauri itapima afya za Wahudumu wa Hoteli, mgahawa, baa, bucha, Machinjio, sehemu za kuokea mikate, nyumba za kulala wageni, grosari au mtu yeyote anayetengeneza chakula kwa ajili ya kuuza na kutoa hati ya afya;

(2) Halmashauri itatoza ada ya ukaguzi wa afya kwa Mujibu wa viwango vitakavyopangwa na kutangazwa na Halmshauri..

Uwezo wa kutoa adhabu ya papo kwa papo

21. (1) Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kutoa adhabu ya papo kwa papo kwa Mtu yeyote atakayechafua mazingira kwa kukiuka taratibu

zilizowekwa na Sheria ndogo hizi na;

(2) endapo adhabu hiyo itahusisha malipo ya faini, Afisa Mwidhiniwa atamkatia Mkosaji stakabadhi ya malipo kutoka Halmashauri.

Makosa

22. Mtu yeyote ambaye-

(a) atamzuia au kujaribu kumzuia Afisa Mwidhiniwa asitekeleze wajibu wake chini ya Sheria Ndogo hizi; au

(b) atatiririsha maji machafu au atamwaga takataka katika mtaa, mtaro wa maji ya mvua, uchochoroni, au mahali popote hadharani au katika eneo lolote la wazi bila idhini ya Halmashauri;

(c) ataendesha biashara ya pombe ndani ya nyumba ya makazi;

(d) ataosha gari, kufua, kunywesha mifugo na kukoroga dawa za mimea ndani ya mito, mabwawa, lambo au ndani ya chanzo maji au kisima kinachotumika kwa matumizi ya binadamu;

(e) atauza vyakula vilivyopikwa bila kufuata taratibu za kiafya zilizowekwa na sheria ndogo hizi;

(f) atafanya matengenezo ya gari, pikipiki na mitambo, kuendesha shughuli za viwanda katika maeneo ya wazi, makazi, barabarani, uchochoroni, au katika maeneo yasiyotengwa kwa shughuli hizo bila kuzingatia taratibu za mipango miji;

(g) ataenda haja ndogo au kubwa hovyo barabarani,

uchochoroni, upenuni au mahali popote ambapo siyo chooni.

(h) atakwenda kinyume na Sheria ndogo hizi

Adhabu

23. Mtu yeyote atakayetenda kosa na kupatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi laki tatu (300,000/=) au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili (12) jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Kufifilisha kosa

24. Mkurugenzi anaweza kumtoza mtu yeyote faini isiyozidi shilingi Elfu Hamsini (50,000/=) iwapo mkosaji atakiri kosa kwa maandishi na kukubali kulipa faini iliyoainishwa chini ya Sheria Ndogo hizi.

JEDWALI LA KWANZA

*(Chini ya kifungu cha 6(2)*

SEHEMU "A"
ADA YA KUZOA TAKA

| NA. | AINA YA JENGO/ BIASHARA | ADA KWA MWEZI |
|---|---|---|
| 1. | Wafanyabiashara wakubwa | 10,000/= |
| 2. | Maduka ya rejareja | 5,000/= |
| 3. | Mgahawa mdogo | 10,000/= |
| 4. | Mgahawa Mkubwa | 5,000/= |
| 5. | Nyumba ya kulala Wageni | 10,000/= |
| 6. | Kiwanda cha mbao | 6,000/= |
| 7. | Fundi Seremala/ Karakana/ Kuchoma vyuma (Mchundo) | 10,000/= |
| 8. | Kiwanda kidogo | 20,000/= |
| 9. | Kiwanda kikubwa | 50,000/= |
| 10. | Bar, klabu za usiku, kumbi za starehe, | 10,000/= |
| 11. | Duka la nyama na samaki | 5,000/= |
| 12. | Duka la Dawa | 5,000/= |
| 13. | Meza za Matunda | 2,500/= |
| 14. | Mama Ntilie, wauza matunda na miwa | 3,000/= |
| 15. | Kituo cha kuuzia mafuta | 10,000/= |
| 16. | Fundi cherehani, Wasusi, Vinyozi | 2,500/= |
| 17. | Wauza Mkaa, klabu za pombe za kienyeji/ asili | 5,000/= |

JEDWALI LA PILI

*(Chini ya kifungu cha 20)*

ADA YA UKAGUZI WA AFYA

| Na. | Aina ya biashara | Kiwango cha ada kwa mwaka |
|---|---|---|
| 1. | Baa na maduka ya vinywaji | 5000/= |
| 2. | Migahawa na Mama Lishe | 2,500/= |
| 3. | Nyumba za Wageni (Guest House) na Hoteli | 10,000/= |
| 4. | Kumbi za starehe au mikutano | 10,000/= |
| 5. | Majengo mengineya Biashara | 5,000/= |

JEDWALI LA TATU

*(Chini ya kifungu cha 11)*

ILANI YA KUONDOA KERO

Ilani hii imetolewa kwa mujibu wa Sheria Ndogo za Usafi wa Mazingira za Halmashauri ya Wilaya ya Malinyi, 2016.

SEHEMU ‘A’

Ndugu…………............... wa Mtaa/Kijiji …………… Kata ya……………Unaarifiwa kwamba katika ukaguzi uliofanyika Tarehe……mwezi………..mwaka…. katika nyumba yako ya Biashara/kuishi iliyopo eneo la……………..kumekutwa machukizo/kero/uchafu kama ifuatavyo;

1) ………………………………………………………………………………..
2) ………………………………………………………………………………..

SEHEMU ‘B’

Kwa **ILANI** hii unaamriwa ndani ya muda wa siku saba (7) tangu siku ya kupokea ilani hii, unatakiwa kutekeleza kwa kuondoa/ kurekebisha/ au kusafisha machukizo/ kero/ uchafu uliotajwa hapo juu; kushindwa kwako kutekeleza ndani ya muda uliopewa Halmashauri italazimika kukuchukulia hatua kali za kisheria bila kulazimika kukupa taarifa.

…………………………………..

**AFISA MUIDHINIWA**

| **IMETOLEWA NA;** | **IMEPOKELEWA NA;** |
|---|---|
| Jina;………………………. | Jina;…………………………. |
| Saini……………………… | saini………………………..... |
| Wadhifa…………………... | wadhifa……………………….. |
| Tarehe…………………….. | Tarehe………………………... |

**Futa lisilohusika*

JEDWALI LA TATU

*(Chini ya kifungu cha 12)*

ILANI YA KUJENGA CHOO

Ilani hii imetolewa kwa mujibu wa Kifungu kidogo cha 32 cha Sheria Ndogo za (Usafi wa Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Malinyi, 2016

SEHEMU ‘A’

Ndugu…………………...............wa Mtaa/Kijiji……………Kata ya…………Unaarifiwa kwamba katika ukaguzi uliofanyika Tarehe……mwezi………..mwaka….Katika nyumba yako ya Biashara/kuishi/kutolea Huduma ya …………………….. iliyopo katika eneo la ………………katika Kitongoji/Mtaa*………. Kijiji cha……………Kata ya………….

Imekutwa haina choo/ choo kimejaa/kimeharibika* hivyo unaamriwa kutekeleza mambo yafuatayo;

(1) ………………………………………………………………………………

(2) ………………………………………………………………………………

SEHEMU ‘B’

Unapewa muda wa siku thelathini (30) tu tangu siku ya kupokea ilani hii kutekeleza maelekezo yote yaliyoelezwa katika sehemu ‘A’ ya Ilani hii,

SEHEMU ‘C’

Ukaguzi wa kuthibitisha utekelezaji wa maelekezo uliyopewa utafanyika tarehe……………….endepo utashindwa kutekeleza maelekezo ndani ya muda uliopewa Halmashauri itakuchukulia hatua kali za kisheria bila kukupa taarifa nyingine.

……………………..
**AFISA MUIDHINIWA**

| | |
|---|---|
| IMETOLEWA NA; | IMEPOKELEWA NA; |
| Jina ;………………………. | Jina ;…………………………. |
| Saini……………………… | saini………………………….... |
| Wadhifa…………………... | wadhifa……………………….. |
| Tarehe…………………….. | Tarehe………………………... |

Nembo ya halmashauri ya Wilaya ya Malinyi imebandikwa kwenye Sheria ndogo hizi kufuatia azimio la Halmashauri iliyotolewa katika kikao kilichofanyika tarehe 23.04.2016 na ilibandikwa mbele ya:-

SAID ALLY MSOMOKA,
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Malinyi.*

FADHILI NASSORO LIGUGUDA,
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya ya Malinyi.*

NAKUBALI,

Dodoma,
09Januari, 2017

GEORGE B. SIMBACHAWENE (MB)
*Waziri wanchi-or-Tamisemi.*